

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**HALMASHAURI YA MANISPAA DODOMA**

*(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)*

**MKOA WA DODOMA**  
Tel.: 2354817/2321550  
Fax: 2321550



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa  
S.L.P.1249  
**Dodoma.**

Barua pepe: md@dodomamc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. HMD/S.20/32/VOL.II/39

Tarehe: 23 Machi, 2018

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Kumb. Na. **CFC.26/205/01'F'/91** cha tarehe 22 Agosti, 2017 kama kilivyoongezewa muda kwa kibali Kumb. Na. **CFC.26/01"GG"/95** cha tarehe 12 Machi, 2018 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma anawatangazia waombaji wenye sifa kujaza nafasi za kazi katika Kada zifuatazo:-

### **1.0 MTENDAJI WA MTAА/KIJIJI DARAJA LA III - NAFASI 30**

#### **1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- (i) Kuwa Katibu wa Kamati ya Mtaa.
- (ii) Kuwa Mtendaji Mkuu wa Mtaa.
- (iii) Mratibu wa Utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa za Halmashauri katika Mtaa.
- (iv) Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa.

- (v) Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaaa
- (vi) Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
- (vii) Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
- (viii) Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote katika Mtaa.
- (ix) Kuandaa na kutunza rejesta za wakazi wote wa Mtaa
- (x) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

## **1.2 MSHAHARA:**

Cheo hiki kina Ngazi ya Mshahara wa - **TGS B.**

## **2.0 MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE**

- i) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri kuanzi miaka 18 na wasiozidi umri wa miaka 45.
- ii) Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
- iii) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- (iv) Picha tatu "Passport size" za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
- (v) "Testimonials", "Provisional results", "Statement of results", Hati ya Matokeo ya Kidato cha nne "result slip" havitakubaliwa.
- (vi) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa tu kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- (vii) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, Kidato cha Nne na cha Sita pamoja na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyohusika.

- (viii) Waombaji wenye vyeti vya Kidato cha Nne na Cheti cha Taaluma ambao vimepatikana Nje ya Nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE).
- (ix) Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.
- (x) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA)
- (xi) Uwasilishaji wa taarifa za kugushi utaadhibiwa kisheria; aidha, maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja Masjala ya Manispaa ya Dodoma au kutumwa kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI WA MANISPAA,  
S. L. P 1249,  
DODOMA.**

- (xii) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 05/04/2018 saa Tisa na nusu (9:30) Alasiri.



Godwin E. Kunambi  
**MKURUGENZI WA MANISPAA  
DODOMA**

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
DODOMA**